

## Unavyoweza Kupata Usaidizi

- **Tupigie simu katika 1.800.889.2047**
- **Pata maelezo kuhusu haki zako za kisheria katika [www.vtlawhelp.org](http://www.vtlawhelp.org)**
- **Tumia Utafutaji wetu wa Usaidizi wa Kisheria wa Mtandaoni ili utafute maelezo ya wavuti, upate ushauri wa kisheria kupitia simu, au utume maombi ya usaidizi wa kisheria mtandaoni katika [www.vtlawhelp.org/triage/vt\\_trage](http://www.vtlawhelp.org/triage/vt_trage)**



**“Kazi nzuri kutoka Vermont Legal Aid. Huduma hailipishwi... Huduma Hii [ni] Nzuri... Hasa kwa wakimbizi, ambao hawajui wanapofaa kuenda na wanapofaa kuzungumza.”**



Burlington | Montpelier | Rutland  
Springfield | St. Johnsbury

**1.800.889.2047**  
[screening@vtlegalaid.org](mailto:screening@vtlegalaid.org)  
[www.vtlawhelp.org](http://www.vtlawhelp.org)  
[www.vtlegalaid.org](http://www.vtlegalaid.org)

## Unahitaji Mkalimani?

احصل على مساعدتنا بلغتك بالاتصال على  
1.800.889.2047  
اخبرنا باسمك ورقم هاتفك ثم انطق العربية.

သင့်ဘာသာစကားမျဖစ် ကြေးနို့မှတ်မဲ့  
အကူအညီရယူရပါ။ 1.800.889.2047 ကိုခေါ်ဆိုပါ။  
သင့်နာမည့်စွဲမှာ ဖုန်းနံပါတ်မှတ်ဆုံး၍ ဝေါ်ခေါ်ပါ။  
မျမှော်(မမှ) ကိုဝေါ်ပါ။

Obtenez de l'aide de nous dans votre langue.  
Appelez 1.800.889.2047. Dites-nous votre  
nom et votre numéro de téléphone. Dites  
français.

हामीबाट आपनै भाषामा सहयोग प्राप्त गर्नुहोस्।  
1.800.889.2047 मा कल गर्नुहोस्। हामीलाई  
तपाईंको नाम र फोन नम्बर भन्नुहोस्। भाषा नेपाली  
भन्नुहोस्।

Caawimo nooga hel anaga luqaddaada. Soo  
wac 1.800.889.2047. Noo sheeg magacaaga  
iyo lambarka talefoonka. Dheh Soomaali.

Reciba nuestra ayuda en su idioma. Llame al  
1.800.889.2047. Díganos su nombre y número  
de teléfono. Diga español.

Pata usaidizi kutoka kwetu kwa lugha yako.  
Piga simu nambari 1.800.889.2047. Tuambie  
jina na nambari yako ya simu. Sema Kiswahili.

Để nhận sự trợ giúp của chúng tôi bằng ngôn  
ngữ của quý vị. Gọi số 1.800.889.2047. Vui  
lòng cho chúng tôi biết tên và số điện thoại  
của quý vị. Vui lòng nói “Tiếng Việt”.



**Vermont Legal Aid**  
Working for Justice



**Usaidizi wa kisheria bila  
malipo kwa wakazi wa  
Vermont wenyewe matatizo ya  
madai ya kisheria yanayotishia  
haki zako, makazi, kazi, afya  
au uzima wako**

**1.800.889.2047**



Vermont Legal Aid ni wakala wa kisheria unaofanya kazi katika jimbo zima, shirika la kibinafsi, na lisilo la faida linalotoa huduma za madai ya kisheria bila malipo. Pia tunatoa maelezo na vifaa vya kujisaidia kupitia tovuti ya Usaidizi wa Kisheria wa Vermont ([vtlawhelp.org](http://vtlawhelp.org)).

Huwa tunawasaidia wakazi wa Vermont wenyе kipato cha chini; watu wazee na watu wenyе umelavu; na mtu yoyote aliye na tatizo linalohusiana na huduma ya afya na bima ya afya.

Huwa hatushughulikii mashtaka ya kijinai.

Huwa hatulipishi huduma zetu. Tunafadhiliwa kupitia michango ya kibinafsi, pamoja na ruzuku za jimbo na shirkisho.

“Nilipowasiliana na nyinyo kwa mara ya kwanza, nilikuwa nimepoteza matumaini yote. Nilikuwa karibu kupata mfadhaiko. Mumebadilisha (na kuokoa) maisha yangu. Kwa hiyo ASANTE kwa yote mulyonifanyia!”

## Unahitaji Usaidizi?

### Piga Simu kwa Vermont Legal Aid

1.800.889.2047

#### Tunachofanya

- **Tunawasaidia wateja wanaoishi katika umasikini.**

*Tunakusaidia kupata manufaa unayohitimu. Tunakusaidia kulinda kipato na manufaa yako kutoka kwa wakusanyaji wa madeni na watu wengine wanaojaribu kuyachukua.*

- **Tunawalinda watu binafsi na familia wanaonyanyaswa na kudhulumiwa.**

*Tunawasaidia wanawake, watoto, watu wenyе ulemavu na watu wazee kuhama maeneo hatari kuishi. Tunakusaidia kulinda haki zako na kuanza maisha yako upya.*

- **Tunajitahidi kulinda haki za wateja za makazi salama, ya bei nafuu.**

*Tunakabiliana na wamiliki nyumba wasiofuata sheria zilizobuniwa kuhakikisha usalama wako na tunahakikisha unatendewa kwa usawa. Tunajaribu kukusaidia kuishi katika nyumba yako.*



- **Tunawasaidia wakazi wa Vermont kuweza kufikia huduma za afya, afya ya kiakili na huduma ya muda mrefu kwa bei nafuu.**

*Tunakusaidia kupata huduma za afya unazohitaji. Ikiwa wewe na mtu mzee au una ulemavu, tunakusaidia kuishi na kupata huduma unazohitaji katika jamii yako.*

- **Tunatekeleza sheria zinazolinda haki zako.**

*Tunajitahidi kuhakikisha unaweza kufikia elimu na makazi. Tunakuwezesha kufanya chaguo zako mwenyewe za maisha.*

**Je, unahitaji usaidizi kutoka kwetu kwa lugha yako?**

**Tuambie.**

**Tutakupatia mkalimani.**